



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA



TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA
WANAFUNZI KATIKA MASWALI YA UPIMAJI WA
KITAIFA WA DARASA LA NNE (SFNA) 2023

MAARIFA YA JAMII



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA



**TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA
WANAFUNZI KATIKA MASWALI YA UPIMAJI WA
KITAIFA WA DARASA LA NNE (SFNA) 2023**

03 MAARIFA YA JAMII

Kimechapishwa na;
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P 2624,
Dar es salaam, Tanzania.

©Baraza la Mitihani la Tanzania, 2024

Haki zote zimehifadhiwa.

YALIYOMO

DIBAJI	iv
1.0 UTANGULIZI	1
2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA KILA SWALI	2
2.1 Sehemu A: Maswali ya Kuchagua na Kuoanisha	2
2.1.1 Swali la 1: Kufuata Kanuni za Kiuchumi Katika Shughuli za Uzalishaji Mali	3
2.1.2 Swali la 2: Kutambua Misingi ya Uzalendo Katika Jamii	11
2.2 Sehemu B: Maswali ya Majibu Mafupi.....	20
2.2.1 Swali la 3: Kutambua Matukio Yanayotokea Katika Mazingira Yanayomzunguka.....	21
2.2.2 Swali la 4: Kutumia Ramani na Elimu ya Anga katika Maisha ya kila Siku	30
3.0 TATHIMINI YA UFAULU KWA KILA UMAHIRI.....	35
4.0 HITIMISHO	36
5.0 MAPENDEKEZO	37
KIAMBATISHO: Ulinganifu wa Ufaulu kwa Wanafunzi katika kila Umahiri kwa Mwaka 2023 na 2022..	38

DIBAJI

Baraza la Mitihani la Tanzania limeandaa taarifa ya uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne kwa somo la Maarifa ya Jamii mwaka 2023. Lengo la taarifa hii ni kutoa mrejesho kwa wanafunzi, walimu, wathibiti ubora wa shule, watunga sera, wakuza mitaala na wadau wengine wa elimu kuhusu kiwango cha ujifunzaji wa wanafunzi katika kipindi cha miaka minne ya elimu ya msingi.

Katika taarifa hii, mambo yaliyochangia ufaulu wa wanafunzi katika kila swali yamebainishwa. Uchambuzi unaonesha kuwa, ufaulu mzuri wa wanafunzi katika maswali ulitokana na uelewa mzuri wa matakwa ya maswali na kuwa na umahiri wa kutosha katika somo. Pamoja na hayo, wanafunzi waliokuwa na ufaulu hafifu katika upimaji huu walikosa maarifa ya msingi ya kutambua matakwa ya maswali. Wanafunzi wengine walikuwa na umahiri wa wastani katika umahiri uliopimwa.

Uchambuzi wa ufaulu wa wanafunzi katika kila umahiri kuonesha kuwa, ufaulu wa wanafunzi ni wa wastani katika umahiri wa *Kutambua Matukio Yanayotokea katika Mazingira Yanayomzunguka, Kufuata Kanuni za Kiuchumi katika Shughuli za Uzalishaji Mali na Kutumia Ramani na Elimu ya Anga katika Maisha ya Kila Siku*. Kwa upande mwingine, umahiri wa *Kutambua Misingi ya Uzalendo katika Jamii* ulikuwa na ufaulu hafifu.

Baraza la Mitihani la Tanzania linatarajia kuwa, mrejesho huu utaziwezesha mamlaka mbalimbali za elimu kuchukua hatua madhubuti ili kuboresha michakato ya ufundushaji na ujifunzaji. Aidha, Baraza linatarajia kuwa, changamoto zilizochangia ufaulu usioridhisha hususan katika umahiri wa *Kutambua Misingi ya Uzalendo katika Jamii* zitatatuliwa ili kuongeza ufaulu kwa wanafunzi wanaotarajia kuingia Darasa la Nne.

Baraza la Mitihani la Tanzania linatoa shukurani za dhati kwa wote walioshiriki katika kuandaa taarifa hii.



Dkt. Said A. Mohamed
KATIBU MTENDAJI

1.0 UTANGULIZI

Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne (SFNA) 2023 ulifanyika Oktoba 2023. Jumla ya wanafunzi 1,693,338 walisajiliwa kufanya upimaji katika somo la Maarifa ya Jamii. Kati yao, wanafunzi 1,545,059 (91.19%) walifanya upimaji, ambapo, wanafunzi 1,340,143 sawa na alisimia 86.75 walifaulu na wanafunzi 204,639 sawa na asilimia 13.25 walipata ufaulu hafifu.

Katika taarifa hii, utangulizi unafuatiwa na uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika kila swali. Uchambuzi unabainisha umahiri uliopimwa, na majibu ya wanafunzi ambayo yamegawanyika katika kiwango kizuri, cha wastani na hafifu. Sababu za ufaulu kwa kila kundi pia zimechambuliwa. Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika kila swali umefuatiwa na tathimini ya ufaulu wa wanafunzi katika kila umahiri. Sehemu hiyo imefuatiwa na hitimisho pamoja na mapendekezo yaliyotokana na uchambuzi uliofanyika.

Viwango vya ufaulu wa wanafunzi vimezingatia asilimia ya ufaulu wa swali husika. Iwapo asilimia ya ufaulu ni 0 hadi 33, kiwango hiki cha ufaulu ni hafifu. Kama asilimia ni 34 hadi 66, ufaulu huo ni wa wastani, na ikiwa asilimia ni 67 hadi 100, kiwango hiki cha ufaulu ni kizuri. Katika taarifa hii, rangi ya kijani, njano na nyekundu zimetumika kuonesha ufaulu mzuri, wastani na hafifu mtawalia.

Karatasi ya Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne katika mwaka 2023 somo la Maarifa ya Jamii ilikuwa na maswali manne. Maswali hayo yaligawanyika katika sehemu kuu mbili A na B. Sehemu A ilikuwa na maswali mawili, swali la 1 na la 2 yenye

jumla ya vipengele 14. Maswali hayo yalitoka katika umahiri mkuu wa *Kufuata Kanuni za Kiuchumi katika Shughuli za Uzalishaji Mali, na Kutambua Msingi ya Uzalendo katika Jamii.*

Sehemu B iliundwa na maswali mawili, swali la 3 na la 4 yenye jumla ya vipengele 11. Maswali hayo yalitoka katika umahiri mkuu wa *Kutambua Matukio Yanayotokea katika Mazingira Yanayomzunguka, na Kutumia Ramani na Elimu ya Anga katika Maisha ya kila Siku.* Wanafunzi walitakiwa kujibu maswali yote kutoka sehemu zote mbili.

2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA KILA SWALI

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi kwa ujumla unaonesha kuwa, kiwango cha ufaulu katika swali la 1, 3 na 4 kilikuwa cha wastani na katika swali la 2 kilikuwa hafifu. Vilevile, vielelezo na chati vimetumika kuonesha majibu ya wanafunzi na takwimu mtawalia.

2.1 Sehemu A: Maswali ya Kuchagua na Kuoanisha


Sehemu hii iliundwa na maswali mawili yenye jumla ya vipengele 14. Swali la 1 lilikuwa na vipengele nane (i) – (viii) vya maswali ya kuchagua jibu sahihi. Katika swali hili wanafunzi walitakiwa kusoma swali na kisha kuchagua jibu sahihi kutoka katika machaguo waliyopewa na kuliandika katika kisanduku kilichoachwa wazi. Swali hili lilikuwa na jumla ya alama 16. Swali la pili lilikuwa na vipengele sita (i) – (vi) vya kuoanisha. Kila mwanafunzi alitakiwa kusoma maswali kutoka fungu A, na kuoanisha na jibu sahihi kutoka fungu B.

2.1.1 Swali la 1: Kufuata Kanuni za Kiuchumi Katika Shughuli za Uzalishaji Mali

Jumla ya wanafunzi 1,545,059 (100%) walijibu swali hili. Aidha, wanafunzi 3,220 (0.21%) walijibu kwa usahihi vipengele vyote nane (8) na kupata alama 16, ambao ni ufaulu mzuri sana. Jumla ya wanafunzi 83,668 (5.41%) walipata alama kuanzia 12 hadi 14 ambao ni ufaulu mzuri kwa kuwa waliweza kujibu kwa usahihi vipengele sita hadi saba katika swali hili.

Kinyume chake, wanafunzi 713,320 (46.16%) walipata alama kuanzia 6 hadi 10 ambao ni ufaulu wa wastani. Kati yao, wanafunzi 125,530 (8.12%) waliweza kujibu kwa usahihi vipengele vitano, wanafunzi 235,896 (15.07%) walijibu kwa usahihi vipengele vinne, na wanafunzi 351,894 (22.77%) waliweza kujibu kwa usahihi vipengele vitatu.

Hata hivyo, wanafunzi 744,851 (48.21%) walikuwa na ufaulu hafifu kwani walipata 0 hadi alama 4. Kati yao, wanafunzi 98,265 (6.36%) hawakujibu kipengele chochote, hivyo walipata 0. Wanafunzi wengine 267,286 (17.30%) walijibu kwa usahihi kipengele kimoja na wengine 379,300 (24.55%) walijibu kwa usahihi vipengele viwili. Kwa ujumla, ufaulu katika swali hili ulikuwa wa wastani kwani wanafunzi 800,208 (51.79%) walipata alama kuanzia 6 hadi 16, kama inavyoonekana kwenye chati Na.1.



Chati Na 1: Ufaulu wa Wanafunzi katika Swali la 1

- (i) Yapi ni mazao ya biashara yanayolimwa Tanzania?
- Mahindi, chai na kahawa
 - Pamba, chai na kahawa
 - Ndizi, kahawa na pamba
 - Mihogo, mpunga na tumbaku

Kipengele hiki cha swali kilimtaka mwanafunzi kubaini mazao ya biashara yanayolimwa Tanzania. Ufaulu katika kipengele hiki ulikuwa mzuri kwani wanafunzi wengi waliweza kuchagua jibu sahihi *B Pamba, chai na kahawa*. Wanafunzi hao walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mazao ya biashara yanayolimwa Tanzania.

Kwa upande mwingine, wanafunzi waliochagua vipotoshi *A Mahindi, chai na kahawa na C, Ndizi, kahawa na pamba*, hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mazao ya biashara yanayolimwa Tanzania. Wanafunzi hawa walipaswa kuelewa

kuwa, mahindi na ndizi ni mazao ya chakula na sio ya biashara. Vilevile, wanafunzi wachache waliochagua kipotoshi *D Mihogo, mpunga na tumbaku*, hawakutambua kuwa, mihogo na mpunga ni mazao ya chakula hivyo yalifanya chaguo hili kutokuwa sahihi.

- (ii) Ipi ni faida ya utalii nchini Tanzania?
- A. Kuiga mila na desturi za wageni
 - B. Kupata fedha za kigeni
 - C. Kuongezeka kwa mazao ya misitu
 - D. Kuongezeka kwa wanyama pori

Kipengele hiki kilimtaka mwanafunzi kubaini faida ya utalii nchini Tanzania. Ufaulu katika kipengele hiki ulikuwa mzuri kwani wanafunzi wengi walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu umuhimu wa utalii hivyo, walichagua jibu sahihi *B Kupata fedha za kigeni*. Wanafunzi hao walitambua kuwa kupitia sekta ya utalii nchi hupata fedha za kigeni kutoka kwa watalii wanaotoka mataifa mengine.

Kinyume na hapo, wanafunzi waliochagua kipotoshi *A Kuiga mila na desturi za wageni*, hawakuwa na maarifa kuwa, sio kila mila na desturi inayoletwa na wageni ni nzuri kuiga. Vivyohivyo, wanafunzi waliochagua kipotoshi *C, Kuongezeka kwa mazao ya misitu*, walishindwa kuelewa kuwa, ongezeko la mazao ya misitu hutokana na utunzaji wa misitu, kupanda miti na utunzaji wa mazingira. Vilevile, baadhi ya wanafunzi walichagua kipotoshi *D Kuongezeka kwa wanyama pori*. Wanafunzi hao walielewa kuwa, kuongezeka kwa wanyama pori ni matokeo ya utunzaji bora wa

wanyama pori lakini hawakuelewa kuwa haihusiani na faida ya utalii Tanzania.

(iii) Madini ya Almasi yana matumizi gani?

- A. Kukatia vioo
- B. Chanzo cha nishati ya joto
- C. Kukatia chuma
- D. Kuzalisha umeme

Katika kipengele hiki mwanafunzi alitakiwa kubaini matumizi ya madini ya Almasi. Ufaulu katika kipengele hiki ulikuwa mzuri kwani wanafunzi wengi waliweza kuchagua jibu sahihi *A Kukatia vioo*. Wanafunzi hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu matumizi ya madini mbalimbali.

Hata hivyo, wanafunzi waliochagua kipotoshi *B Chanzo cha nishati ya joto*, hawakuelewa kuwa, chanzo cha nishati ya joto hujumuisha mafuta, mwanga wa jua na umeme ambavyo havina uhusiano na matumizi ya almasi. Vilevile, wanafunzi waliochagua kipotoshi *C Kukatia chuma*, hawakuelewa kuwa, chuma hukatwa na misumeno au kwa kuyeyushwa kwenye moto. Vivyohivyo, wanafunzi waliochagua kipotoshi *D Kuzalisha umeme*, hawakutambua kuwa, umeme huzalishwa kwa njia ya maji, jua, upepo na madini ya urania. Hivyo, kufanya uchaguzi wa vipotoshi B, C, na D kutokuwa sahihi katika swali hili.

(iv) Mbuga ipi ni kubwa kuliko zote nchini Tanzania?

- A. Ruaha
- B. Ngorongoro
- C. Mikumi
- D. Serengeti

Kipengele hiki kilimtaka mwanafunzi kubaini mbuga kubwa kuliko zote nchini Tanzania. Ufaulu katika kipengele hiki ulikuwa mzuri kwani wanafunzi wengi waliweza kuchagua jibu sahihi *A Ruaha*. Uchaguzi wa jibu hili unadhihirisha kuwa wanafunzi hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu Mbuga za Wanyama zinazopatikana Tanzania, na ukubwa wake. Hivyo, walibaini kuwa mbuga kubwa kuliko zote ni Ruaha inayokadiriwa kuwa na ukubwa wa kilometa za eneo la mraba 20,226.

Kwa upande mwingine, wanafunzi wengine walichagua vipotoshi *B Ngorogoro*, *C Mikumi* na *D Serengeti*. Wanafunzi hao hawakuelewa kuwa Ngorongoro inakadiriwa kuwa na eneo la ukubwa wa kilometa za mraba 8,292, Mikumi inakadiriwa kuwa na eneo la ukubwa wa kilometa za mraba 3,230 na Serengeti ina eneo la ukubwa wa kilometa za mraba 14,750. Hivyo, kufanya Ruaha kuwa mbuga kubwa Tanzania.

- (v) Bainisha wanyama wanaofugwa kati ya wafuatao:
- A. simba, ng'ombe na kondoo
 - B. pundamilia, kondoo na chui
 - C. twiga, kondoo na mbuzi
 - D. mbwa, kondoo na mbuzi

Kipengele hiki kilimtaka mwanafunzi kubaini wanyama wanaofugwa. Ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri ambapo wanafunzi wengi waliweza kuchagua jibu sahihi *D mbwa, kondoo na mbuzi*. Wanafunzi hao walionesha uelewa mzuri kuhusu wanyama, wafugwao nyumbani.

Kwa upande mwingine, wanafunzi waliochagua vipotoshi; *A simba, ng'ombe na kondoo, B pundamilia, kondoo na chui na C twiga, kondoo na mbuzi* hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu wanyama wafugwao. Wanafunzi hao walipaswa kuelewa kuwa, vipotoshi A, B na C vilijumuisha wanyama wasiofugwa kama; simba, pundamilia, chui na twiga. Hivyo, kufanya uchaguzi wao kutokuwa sahihi.

(vi) Ipi ni njia sahihi ya kutunza misitu?

- A. Kuchoma miti ili kupunguza msongamano
- B. Kuzalisha mkaa ili kuongeza kipato
- C. Kupanda miti mingine baada ya kukata ya awali
- D. Kujenga maeneo ya misitu ili kupata hewa safi

Katika kipengele hiki mwanafunzi alitakiwa kubaini njia sahihi ya kutunza misitu. Ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa mzuri, kwani wanafunzi wengi waliweza kuchagua jibu sahihi *C kupanda miti mingine baada ya kukata ya awali*. Jibu hili linadhihirisha kwamba wanafunzi hao walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu njia mbalimbali za kuhifadhi mazingira, hususani utunzaji wa misitu.

Mbali na hayo, wanafunzi wengine waliochagua kipotoshi *A Kuchoma miti ili kupunguza msongamano*. Wanafunzi hawa hawakutambua kuwa, uchomaji wa miti huharibu miti midogo na mikubwa. Vilevile, wanafunzi waliochagua kipotoshi *B Kuzalisha mkaa ili kuongeza kipato*, hawakuelewa kuwa, uchomaji wa

mkaa unahusisha ukataji wa miti hivyo huharibu misitu badala ya kutunza. Pia, wanafunzi waliochagua kipotoshi *D Kujenga maeneo ya misitu ili kupata hewa safi*, hawakuelewa kuwa, kujenga maeneo hayo husababisha shughuli mbalimbali za kibinadamu kama vile kilimo, ufugaji, kutengeneza mbao na kukata miti kama chanzo cha nishati ambazo huchangia kuharibu misitu.

- (vii) Ni madini yapi hutumika kutengeneza saruji?
- A. Chuma
 - B. Chokaa
 - C. Fosfeti
 - D. Chumvi

Mwanafunzi alitakiwa kubaini madini yanayotumika kutengeneza saruji. Ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa mzuri kwani wanafunzi wengi waliweza kuchagua jibu sahihi *B Chokaa*. Hii inathibitisha kwamba wanafunzi hao walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu matumizi ya madini mbalimbali.

Kinyume chake, wanafunzi waliochagua kipotoshi *A Chuma*, walikosa maarifa kuhusu madini haya. Wanafunzi hao walipaswa kuelewa kuwa chuma hutumika kutengenezea miundombinu, mashine na vifaa mbalimbali, vifaa vya kupikia na uzalishaji wa bidhaa zitumikazo nyumbani.

Hata hivyo, wanafunzi waliochagua kipotoshi *C Fosfeti*, hawakuwa na ufahamu kuwa, fosfeti hutumika kutengeneza mbolea. Vilevile, wanafunzi waliochagua kipotoshi *D Chumvi*,

hawakuweza kubaini kuwa, chumvi hutumika katika mapishi na utunzaji wa vyakula. Hivyo, kufanya uchaguzi wa vipotoshi A, C na D kutokidhi vigezo vya kuwa jibu sahihi.

- (viii) Kwa nini kilimo ni uti wa mgongo kwa uchumi wa Tanzania?
- A. Huvutia watalii wengi nchini
 - B. Watu wengi wameajiriwa kwenye kilimo
 - C. Watu wengi huishi mashambani
 - D. Wawekezaji wengi wamewekeza kwenye kilimo

Kipengele hiki kilimtaka mwanafunzi kubaini sababu za kilimo kuwa uti wa mgongo kwa uchumi wa Tanzania. Ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa mzuri, kwani wanafunzi wengi walichagua jibu sahihi *B, watu wengi wameajiriwa kwenye kilimo*. Wanafunzi hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu shughuli za uzalishaji mali, kwani waliweza kubaini kuwa watu wengi nchini Tanzania hujihusisha na kilimo.

Kwa upande mwingine, wanafunzi waliochagua kipotoshi *A, huvutia watalii wengi nchini*, hawakuelewa kuwa, watalii huja nchini kwa kuvutiwa na vivutio vya utalii kama vile; mbuga za wanyama, hifadhi za Taifa, milima, mabonde, misitu, maziwa, bahari na mito. Vilevile, wanafunzi waliochagua kipotoshi *C, watu wengi huishi mashambani*, hawakuwa na uelewa kuwa, kitendo cha watu wengi kuishi mashambani hakimfanyi mtu ategemee kilimo. Kuna watu wengi wanaishi mashambani lakini

hawajihusishi na shughuli za kilimo bali baadhi yao ni wafanyabiashara, watafiti na watumishi wa Umma. Wanafunzi wengine waliochagua kipotoshi *D wawekezaji wengi wamewekeza kwenye kilimo*, walidhihirisha kuwa na uelewa mdogo kuhusu wawekezaji, kwani sio kweli kwamba, wawekezaji wengi wamewekeza katika sekta ya kilimo tu bali kuna wawekezaji wengi nchini ambao wamewekeza katika sekta nyingine kama vile; utalii, uvuvi, madini, viwanda, benki, taasisi za elimu na taasisi za afya.


2.1.2 Swali la 2: Kutambua Misingi ya Uzalendo Katika Jamii

Swali hili lilitoka katika umahiri mkuu wa *Kutambua Misingi ya Uzalendo Katika Jamii* na umahiri mahususi wa *Kuwaenzi Mashujaa Wetu*. Katika swali hili mwanafunzi alitakiwa kuoanisha mchango wa mashujaa katika fungu A na majina yao katika fungu B. Wanafunzi walitakiwa kuandika herufi ya jibu sahihi kwenye mabano waliyopewa. Swali hili liliwapima wanafunzi uwezo wa kutambua mchango wa mashujaa wa Tanzania. Swali hili lilikuwa na jumla ya alama 12. Swali lilikuwa kama ifuatavyo: Jibu kipengele cha (i) – (vi) kwa kuoanisha mchango wa mashujaa wa Tanzania katika Fungu A na majina yao katika Fungu B. Andika herufi ya jibu sahihi kwenye mabano uliyopewa.

Fungu A	Herufi	Fungu B
(i) Aliwaongoza Waafrika kupinga uvamizi wa Wajerumani katika eneo la Kilwa Kivinje mwaka 1890	(.....)	A. Mtemi Machemba B. John P. Magufuli C. Abushiri bin Sultani
(ii) Alianzisha sera ya soko huria	(.....)	D. Benjamin W. Mkaapa
(iii) Aliwaongoza Wazigua kupinga uvamizi wa Kijerumani katika eneo la Tanga mwaka 1890	(.....)	E. Bwana Heri F. Ali H. Mwinyi G. Julius K. Nyerere H. Hasan bin Omary Makunganya
(iv) Alitekeleza sera ya elimu bure kwa wote kuanzia Darasa la Awali hadi Kidato cha Nne	(.....)	
(v) Aliwaongoza Wayao wa Masasi na Tunduru kupigana na Wajerumani mwaka 1890	(.....)	
(vi) Alianzisha mfumo wa ubinafsishaji	(.....)	

Swali hili lilijibiwa na wanafunzi 1,545,059 (100%) kati ya wanafunzi hao 1,084,808 (70.22%) walikuwa na ufaulu hafifu kwani walipata 0 hadi alama 2. Hata hivyo, wanafunzi wengine 373,428 (24.16%) walipata alama 4 hadi 6 ambao ni ufaulu wa

wastani. Vilevile, Wanafunzi 75,606(4.89%) walipata alama 8 hadi 10 ambao ni ufaulu mzuri. Kwa upande mwingine wanafunzi 11,217 (0.72%) walipata alama zote 12 ambao ni ufaulu mzuri sana. Kwa ujumla ufaulu katika swali hili ulikuwa hafifu kwani ni wanafunzi 460,251 (29.79%) tu ndio waliopata alama kuanzia 4 hadi 12.



Chati Na. 2: *Ufaulu wa Wanafunzi katika Swali la 2*

Uchambuzi zaidi wa majibu ya wanafunzi unadhihirisha kuwa, wanafunzi 11,217 (0.72%) waliojibu vipengele vyote sita kwa usahihi, na kupata alama zote 12 katika swali hili, walikuwa na umahiri wa kutosha kuhusu *Kuwaenzi Mashujaa Wetu*. Wanafunzi hawa walikuwa na uwezo mzuri wa kuoanisha majina ya Mashujaa na michango yao kwa maendeleo ya Tanzania. Kielelezo Na.1.1 kinadhihirisha sampuli ya majibu sahihi ya mwanafunzi katika Swali la 2.

2. Jibu kipengele cha (i) - (vi) kwa kuoanisha mchango wa mashujaa wa Tanzania katika **Fungu A** na majina yao katika **Fungu B**. Andika herufi ya jibu sahihi kwenye mabano uliyopewa.

Fungu A	Herufi	Fungu B
(i) Aliwaongoza Waafrika kupinga uvamizi wa Wajerumani katika eneo la Kilwa Kivinje mwaka 1890.	(H)	A. Mtemi Machemba
(ii) Alianzisha sera ya soko huria.	(F)	B. John P. Magufuli C. Abushiri bin Sultani
(iii) Aliwaongoza Wazigua kupinga uvamizi wa Kijerumani katika eneo la Tanga mwaka 1890.	(E)	D. Benjamin W. Mkapa
(iv) Alitekeleza sera ya elimu bure kwa wote kuanzia Darasa la Awali hadi Kidato cha Nne.	(B)	E. Bwana Heri
(v) Aliwaongoza Wayao wa Masasi na Tunduru kupigana na Wajerumani mwaka 1890.	(A)	F. Ali H. Mwinyi G. Julius K. Nyerere
(vi) Alianzisha mfumo wa ubinafsishaji.	(D)	H. Hasan bin Omari Makunganya

Kielelezo Na.1.1: Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyejibu kwa usahihi vipengele vyote sita vya swali la 2

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, wanafunzi walipata alama zote 12 katika swali la 2, kwa sababu walielewa vizuri matakwa ya swali katika kila kipengele kama ifuatavyo;

Katika kipengele cha (i), mwanafunzi alitakiwa kutambua shujaa aliyewaongoza Waafrika kupinga uvamizi wa Wajerumani katika eneo la Kilwa Kivinje mwaka 1890. Jibu sahihi lilikuwa ni H,

Hasan bin Omari Makunganya. Jibu hili lilijibiwa na wanafunzi wenye maarifa ya kutosha kuhusu viongozi wa Afrika waliotawala Kilwa Kivinje, hususani aliyewapinga Wajerumani mwaka 1890. Kwa upande mwingine, wanafunzi waliooanisha kipengele hiki na kipotoshi *A Mtemi Mchemba*, walishindwa kubaini kuwa, kiongozi huyo aliwaongoza Wayao wa Masasi na Tunduru kupigana na Wajerumani mwaka 1890. Vilevile, wanafunzi waliooanisha na kipotoshi *C Abushiri bin Sultani*, hawakuelewa kuwa aliwangoza watu wa Pwani kupigana dhidi ya Wajerumani kati ya mwaka 1888-1889. Vita hivyo vilipiganwa maeneo ya Pwani kuanzia Tanga (Pangani) hadi Lindi na Mikindani. Vivyo hivyo, wanafunzi waliooanisha na kipotoshi *E, Bwana Heri*, hawakuwa na maarifa ya kutosha juu ya kiongozi aliyewaongoza Wazigua kupinga uvamizi wa Kijerumani katika eneo la Tanga mwaka 1890.

Kipengele cha (ii) kilimtaka mwanafunzi kumtambua shujaa aliyeanzisha sera ya soko huria nchini Tanzania. Jibu sahihi lilikuwa *F, Ali H. Mwinyi*, ambalo lilijibiwa na wanafunzi wenye maarifa ya kutosha kuhusu *mashujaa wa Tanzania na michango yao katika jamii*. Kinyume chake, wanafunzi wengine waliooanisha kipengele hiki na kipotoshi *B, John P. Magufuli*. Wanafunzi hao walipaswa kuelewa kwamba kiongozi huyo hakuanzisha sera ya soko huria bali alitekeleza sera ya elimu bure kwa wote kuanzia Darasa la Awali hadi Kidato cha Nne. Hata hivyo, wanafunzi wachache waliooanisha kipengele hiki na kipotoshi *G, Julius K Nyerere*, wanafunzi hao walipaswa kuelewa

kuwa, Mwl Julius K. Nyerere alianzisha sera ya Ujamaa na Kujitegemea na sio sera ya ubinafsishaji.

Katika kipengele cha (iii), mwanafunzi alitakiwa kutambua kiongozi aliyewaongoza Wazigua kupinga uvamizi wa Kijerumani katika eneo la Tanga mwaka 1890. Jibu sahihi lilikuwa *E, Bwana Heri*, ambalo lilijibiwa na wanafunzi wenye uelewa thabiti kuhusu viongozi wa Wazigua. Kinyume chake, wanafunzi waliojibu kwa kuandika kipotoshi, *H, Hasan bin Omari Makunganya*, hawakuelewa kuwa kiongozi huyu aliwaongoza Waafrika kupinga uvamizi wa Wajerumani katika eneo la Kilwa Kivinje mwaka 1890. Hata hivyo, wanafunzi walioanisha kipengele hiki na kipotoshi *A, Mtemi Mchemba*, hawakuelewa kuwa, kiongozi huyu aliwaongoza Wayao wa Masasi na Tunduru kupigana na Wajerumani mwaka 1890.

Vilevile, wanafunzi walioanisha kipengele hiki na kipotoshi *C, Abushiri bin Sultani*, hawakutambua kuwa, Abushiri bin Sultani aliwaongoza watu wa pwani kupinga uvamizi dhidi ya Wajerumani kati ya mwaka 1888-1889. Vita hivyo vilipiganwa maeneo ya pwani kuanzia Tanga (Pangani) hadi Lindi na Mikindani.

Katika kipengele cha (iv), mwanafunzi alitakiwa kubaini shujaa aliyetekeleza sera ya elimu bure kwa wote kuanzia Darasa la Awali hadi kidato cha Nne. Jibu sahihi lilikuwa, *B, John P. Magufuli*. Jibu hili lilijibiwa na wanafunzi wenye maarifa ya kutosha kuhusu mchango wa shujaa huyo ambaye alikuwa Rais

wa awamu ya tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wanafunzi hao walikuwa na uelewa kuwa kiongozi huyu ndiye aliyetekeleza sera ya elimu bure kwa wote kuanzia Darasa la Awali hadi kidato cha Nne. Kwa upande mwingine, wanafunzi walioanisha kipengele hiki na kipotoshi *F, Ali H. Mwinzi*, hawakuelewa kuwa shujaa huyo, aliyekuwa Rais wa awamu ya pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alianzisha sera ya soko huria na sio elimu bure kuanzia darasa la awali hadi kidato cha nne.

Vilevile, wanafunzi wengine walioanisha kipengele hicho na kipotoshi *G, Julius K Nyerere*. Wanafunzi hao hawakuelewa kuwa Mwl Julius K. Nyerere, Rais wa kwanza wa Tanzania ndiye aliyeeongoza harakati za kupigania uhuru na kuanzisha sera ya Ujamaa na Kujitegemea. Hata hivyo, wanafunzi wengine walioanisha kipengele hiki kwa kuandika kipotoshi *D, Benjamini W Mkapa*. Wanafunzi hao hawakuelewa kuwa rais Benjamini W Mkapa aliyekuwa Rais wa awamu ya tatu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alianzisha mfumo wa ubinafsishaji nchini Tanzania na sio sera ya elimu bure kwa wote kuanzia darasa la awali hadi kidato cha nne.

Katika kipengele cha (v), mwanafunzi alitakiwa kubaini shujaa aliyewaongoza Wayao wa Masasi na Tunduru kupigana na Wajerumani mwaka 1890. Jibu sahihi lilikuwa ni *A, Mtemi Mchemba*. Jibu hili liliandikwa na wanafunzi wenye maarifa ya kutosha kuhusu mashujaa wa mwanzo wa Tanzania. Wanafunzi hao walielewa kuwa Mtemi Mchemba aliunda kikundi cha

kupigana dhidi ya Wajerumani katika eneo lake mwaka 1890. Aidha, wanafunzi waliooanisha kipengele hiki na kipotoshi C, *Abushiri bin Sultani*, hawakuelewa kuwa shujaa huyo alipinga uvamizi dhidi ya Wajerumani maeneo ya Pwani kuanzia Pangani hadi Lindi na Mikindani. Pia, wanafunzi waliojibu kipengele hiki kwa kuoanisha na kipotoshi E, *Bwana Heri*, walikosa maarifa kuwa, kiongozi huyo aliwaongoza Wazigua kupinga uvamizi dhidi ya Wajerumani katika eneo la Tanga mwaka 1890. Vivyo hivyo, wanafunzi waliojibu kipengele hiki kwa kuchagua kipotoshi, H, *Hasan bin Omari Makunganya*, hawakuelewa kuwa kiongozi huyo aliwaongoza Waafrika kupinga uvamizi dhidi ya Wajerumani katika eneo la Kilwa Kivinje mwaka 1890.

Kipengele cha (vi) kilimtaka mwanafunzi kubaini kiongozi aliyeanzisha mfumo wa ubinafsishaji. Jibu sahihi lilikuwa D, *Benjamini W Mkapa*. Jibu hili liliandikwa na wanafunzi wenye uelewa wa kutosha juu ya michango ya Marais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wanafunzi hao walitambua kuwa, Benjamini W. Mkapa alikuwa Rais wa awamu ya tatu aliyeanzisha Mfumo wa ubinafsishaji. Kwa upande mwingine, wanafunzi waliooanisha kipengele hiki na kipotoshi B, *John P. Magufuli*, hawakutambua kuwa huyu alikuwa Rais wa awamu ya tano wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania aliyetekeleza sera ya elimu bure kwa wote kuanzia Darasa la Awali hadi kidato cha Nne. Vilevile, wanafunzi waliooanisha kipengele hiki na kipotoshi F, *Ali H. Mwinyi*, walishindwa kuelewa kuwa huyu alikuwa Rais aliyeanzisha sera ya soko huria. Vivyo hivyo, wanafunzi wengine

walioanisha kipengele hiki na kipotoshi G, *Julius K Nyerere*, wanafunzi hao walipaswa kuelewa kuwa, Mwl Julius K. Nyerere, Rais wa kwanza wa Jamhuri ya muungano wa Tanzania alihamasisha kupigania uhuru wa Tanganyika na alishiriki katika kuanzishwa kwa muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Pia alianzisha sera ya Ujamaa na Kujitegemea na elimu bure kwa wote.

Hata hivyo, wanafunzi waliopata 0 hawakuwa na maarifa kuhusu michango ya mashujaa wa Tanzania kwa ustawi wan chi yetu. Wanafunzi hao walioanisha kimakosa michango ya mashujaa wa Tanzania na majina yao. Hii inathibitisha kuwa, wanafunzi hao hawakuelewa matakwa ya swali au walishindwa kuhusianisha michango ya mashujaa wa Tanzania na majina yao. Kielelezo Na. 1.2 kinaonesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya mwanafunzi ambaye alishindwa kuoanisha vipengele vyote katika swali hili.

2. Jibu kipengele cha (i) - (vi) kwa kuoanisha mchango wa mashujaa wa Tanzania katika **Fungu A** na majina yao katika **Fungu B**. Andika herufi ya jibu sahihi kwenye mabano uliyopewa.

Fungu A	Herufi	Fungu B
(i) Aliwaongoza Waafrika kupinga uvamizi wa Wajerumani katika eneo la Kilwa Kivinje mwaka 1890.	(D)	A. Mtemi Machemba
(ii) Alianzisha sera ya soko huria.	(C)	B. John P. Magufuli C. Abushiri bin Sultani
(iii) Aliwaongoza Wazigua kupinga uvamizi wa Kijerumani katika eneo la Tanga mwaka 1890.	(A)	D. Benjamin W. Mkapa
(iv) Alitekeleza sera ya elimu bure kwa wote kuanzia Darasa la Awali hadi Kidato cha Nne.	(E)	E. Bwana Heri
(v) Aliwaongoza Wayao wa Masasi na Tunduru kupigana na Wajerumani mwaka 1890.	(G)	F. Ali H. Mwinyi G. Julius K. Nyerere
(vi) Alianzisha mfumo wa ubinafsishaji.	(H)	H. Hasan bin Omari Makunganya

Kielelezo Na. 1.2: *Sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya mwanafunzi ambaye alishindwa kuoanisha vipengele vyote katika swali la 2*

2.2 Sehemu B: Maswali ya Majibu Mafupi

Sehemu hii ilikuwa na maswali mawili ya majibu mafupi, swali la 3 na la 4. Katika swali la 3 mwanafunzi alitakiwa kusoma kifungu cha habari kisha kujibu maswali yanayotokana na kifungu hicho. Swali hili lilikuwa na vipengele saba vilivyokuwa na alama 2 kila kimoja hivyo kufanya jumla ya alama 14. Katika swali la 4, mwanafunzi alitakiwa kuchora alama nne za ramani. Kila kipengele kilikuwa na alama 2, hivyo jumla ya alama katika swali la 4 zilikuwa 8. Hivyo, uchambuzi zaidi unaonesha kuwa ufaulu katika swali la 3 na la 4 ulikuwa wa wastani.

2.2.1 Swali la 3: Kutambua Matukio Yanayotokea Katika Mazingira Yanayomzunguka

Swali hili lilitoka katika umahiri mkuu wa *Kutambua Matukio Yanayotokea Katika Mazingira Yanayomzunguka*, na umahiri mahususi wa *Kutunza Mazingira ya Jamii Inayomzunguka*. Katika swali hilo, mwanafunzi alitakiwa kusoma habari kuhusu Utunzaji wa Mazingira ya Shule, kisha kujibu vipengele vilivyoulizwa kwa kuandika jibu sahihi katika nafasi zilizoachwa wazi.

Mwanafunzi alitakiwa kujibu vipengele vyote saba vya swali hili, ambavyo ni (a) hadi (g). Katika kipengele (a) mwanafunzi alipimwa kutambua umuhimu wa kuishi katika mazingira safi, kipengele (b) kilimtaka mwanafunzi kubaini kiumbe hai chenye kudhuru watu na wanyama, kipengele (c) kilimtaka mwanafunzi kutaja kifaa cha usafi, kipengele (d) kilimtaka mwanafunzi kubaini ugonjwa unaoweza kudhibitiwa kwa kufyeka nyasi na kuondoa maji yaliyotuama, kipengele (e) mwanafunzi alitakiwa kubaini mdudu anayesababisha kipindupindu, kipengele (f) mwanafunzi alitakiwa kubaini mazingira ambayo wadudu na wanyama hatarishi hupatikana. Vilevile, katika kipengele (g) mwanafunzi alitakiwa kutambua namna ambayo tunaweza kuwa na mazingira safi. Kielelezo Na. 2.1 kinaonesha habari iliyotumika katika swali hili.

3. Soma kifungu cha habari kifuatacho kisha jibu maswali yanayofuata kwa kuandika jibu sahihi katika nafasi iliyoachwa wazi.


Shule yetu ina mazingira safi. Mazingira machafu ni maficho ya wadudu na wanyama hatarishi kama inzi, mbu, panya na nyoka. Kati ya viumbe hao, nyoka ni hatari zaidi kwa kuwa sumu yake ina madhara makubwa kwa binadamu na wanyama wengine. Ni muhimu kuishi katika mazingira safi.

Mazingira safi hupunguza kuenea kwa magonjwa mbalimbali kama malaria na kipindupindu. Malaria huenezwa na mbu wanaoishi katika majani marefu na maji yaliyotuama. Kipindupindu husababishwa na inzi wanaoishi kwenye majani marefu. Magonjwa hayo yanaweza kuepukika kwa kufyeka nyasi na kufukia mashimo yenye maji ili maji yasisitame. Mazingira safi pia hutusaidia kupata hewa safi ya oksijeni. Ili kuhakikisha kuwa mazingira yetu yanaendelea kuwa safi, ni lazima tufanye usafi wa mazingira kila siku kwa kutumia jembe na fyekeo.

Kielelezo Na. 2.1: *Kifungu cha habari ambacho wanafunzi walitakiwa kusoma na kisha kujibu swali la 3*

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, swali hili lilijibiwa na jumla ya wanafunzi 1,545,059 (100%). Kati yao, wanafunzi 239,614 (14.27%) walipata alama zote 14 ambao ni ufaulu mzuri sana. Wanafunzi hao walikuwa na maarifa ya kutosha kwani walijibu vipengele vyote 7 kwa usahihi. Wanafunzi wengine 472,015 (30.72%) walipata alama 10 hadi 12 ambao ni ufaulu mzuri. Wanafunzi hao walijibu kwa usahihi vipengele 5 hadi 6. Kwa upande mwingine, wanafunzi 320,859 (21.31%) walipata alama 6 hadi 8 ambao ni ufaulu wa wastani. Hata hivyo, wanafunzi

512,571 (33.70%) walipata 0 hadi alama 4 ambao ni ufaulu hafifu. Wanafunzi hao hawakujibu kipengele chochote au walijibu kwa usahihi kipengele 1 au 2. Kwa ujumla, ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa wa wastani kwani jumla ya wanafunzi 1,032,488 (66.83%) walipata kuanzia alama 6 hadi 14. Chati Na. 3 inaonesha kiwango cha ufaulu wa wanafunzi katika swali hili.



Chati Na. 3: *Ufaulu wa Wanafunzi katika swali la 3*

(a) Kwa nini ni muhimu kuishi katika mazingira safi?

Kipengele hiki kilimtaka mwanafunzi kubaini umuhimu wa kuishi katika mazingira safi. Ufaulu katika kipengele hiki ulikuwa mzuri kwani wanafunzi wengi waliweza kubaini umuhimu wa kuishi katika mazingira safi kuwa *hupunguza kuenea kwa magonjwa*

mbalimbali. Huu ni uthibitisho kuwa wanafunzi hao walisoma na kuelewa vizuri maudhui ya kifungu cha habari.

Kinyume chake, baadhi ya wanafunzi waliandika majibu kama vile; *shule yetu ina mazingira safi, mazingira machafu ni maficho ya wadudu na wanyama*, wanafunzi hao hawakuwa na maarifa ya kutosha katika usomaji wa kifungu cha habari. Sambamba na hilo, wanafunzi wachache waliandika sentensi, majina ya wadudu kama vile, nzi na mbu pamoja na wanyama kama vile panya na simba ambayo si majibu sahihi. Majibu hayo yanathibitisha kuwa wanafunzi hao hawakuwa na stadi ya kusoma kwa ufahamu kwani walishindwa kuelewa maudhui ya habari.

(b) Ni kiumbe hai kipi ambacho kina sumu na huweza kudhuru watu na wanyama wengine?

Mwanafunzi alitakiwa kubaini kiumbe chenye sumu kinachoweza kudhuru watu na wanyama. Ufaulu katika kipengele hiki ulikuwa mzuri, kwani wanafunzi wenye umahiri mzuri waliweza kujibu kwa ufasaha kwa kuandika *Nyoka*. Wanafunzi hao waliweza kubaini kuwa nyoka anasumu inayoweza kudhuru watu na Wanyama wengine.

Kwa upande mwingine, wanafunzi waliopata sifuri walitoa majibu yasiyo sahihi kwa kuandika wanyama na wadudu kama vile; *inzi, mbu* na *panya*. Majibu hayo yanathibitisha kuwa wanafunzi katika kundi hili hawakuelewa matakwa ya swali hivyo waliandika majina ya wanyama na wadudu ambao wametajwa kwenye habari.

- (c) Kwa kuzingatia kifungu cha habari, taja kifaa kimoja kinachotumika kufanya usafi.

Kipengele hiki kilimtaka mwanafunzi kutaja kifaa cha usafi. Ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri ambapo wanafunzi wengi waliweza kutaja kwa usahihi vifaa vinavyotumika katika usafi kuwa ni *jembe* au *fyekeo*. Hata hivyo, baadhi ya wanafunzi waliandika majibu yasiyo sahihi kama vile; *hewa safi ya oksijeni*, *ufagio* na *reki*. Majibu hayo yanaashiria kwamba wanafunzi hawakuelewa matakwa ya swali kwani wamenakili baadhi ya maneno au sentensi kutoka kwenye kifungu cha habari au wameandika majibu ambayo hayahusiani na habari

- (d) Ni ugonjwa gani unaweza kuepukwa kwa kufyeka nyasi na kuondoa maji yaliyotuama?

Katika kipengele hiki mwanafunzi alitakiwa kubaini ugonjwa unaoweza kudhibitiwa kwa kufyeka nyasi na kuondoa maji yaliyotuama. Ufaulu katika kipengele hiki ulikuwa mzuri kwani wanafunzi wenye umahiri mzuri kuhusu magonjwa mbalimbali walijibu kwa usahihi kwa kuandika; *Malaria*. Jibu hili, inaonesha kwamba wanafunzi hao walikuwa na umahiri wa kutosha katika kusoma habari na kubaini ujumbe uliomo. Hata hivyo, walikuwa na uelewa wa kutosha namna utunzaji wa mazingira unavyoweza kutukinga dhidi ya magonjwa.

Kwa upande mwingine, baadhi ya wanafunzi katika swali hili waliandika majibu kama vile; *uchafu, mazingira safi, hewa safi, nyoka na panya*. Wanafunzi hao walishindwa kuelewa matakwa ya swali na kuandika majibu ambayo sio sahihi. Majibu haya yanathibitisha kwamba wanafunzi hawa hawakuwa na ujuzi wa kusoma kwa ufahamu.

(e) Mdudu yupi anaweza kusababisha kuenea kwa ugonjwa wa kipindupindu?

Kipengele hiki kilimtaka mwanafunzi kubaini mdudu anayesababisha ugonjwa wa kipindupindu. Ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri kwani, wanafunzi wengi walijibu kwa kuandika jibu sahihi ambalo ni *inzi*. Wanafunzi hao walibaini kuwa *inzi* ndio mdudu anayeeneza ugonjwa wa kipindupindu. Hii inathibitisha kuwa walielewa habari pia walikuwa na maarifa kuhusu namna magonjwa mbalimbali yanavyo ambukizwa.

Kwa upande mwingine, baadhi ya wanafunzi walikuwa na ufaulu hafifu katika kipengele hiki kwani walishindwa kubaini kuwa, mbu hueneza ugonjwa wa malaria na sio kipindupindu. Vilevile, baadhi ya wanafunzi katika kundi hili waliandika *nyoka* na wengine waliandika *panya*. Wanafunzi hao walipaswa kuelewa kuwa *inzi* ni mdudu anayeeneza ugonjwa wa kipindupindu na sio malaria. Pia, *nyoka* na *panya* sio wadudu na hawaenezi malaria.

(f) Kutokana na habari uliyoisoma, wadudu na wanyama hatarishi hupatikana wapi?

Kipengele hiki cha swali kilimtaka mwanafunzi kubaini mazingira ambayo wadudu na wanyama hatarishi wanaweza kupatikana. Ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri kwani wanafunzi wengi walitambua kuwa wanyama na wadudu hatarishi huishi katika mazingira machafu. Majibu haya yanathibitisha kwamba wanafunzi hao walikuwa na ujuzi wa kusoma na kuelewa kifungu cha habari.

Hata hivyo, baadhi ya wanafunzi hawakuelewa matakwa ya kipengele hivyo kuandika majibu yasiyo sahihi kama vile; *shule*. Wanafunzi hao hawakuelewa kuwa, shule ni sehemu maalum ya wanafunzi kujifunza na kufundishwa na walimu wao. Vilevile, wanafunzi wachache walioandika *nyumbani*, kama jibu sahihi. Wanafunzi hao walipaswa kuelewa kuwa nyumbani ni sehemu ambayo watu huishi sio makazi ya wadudu na wanyama hatarishi. Majibu haya ni uthibitisho kuwa, wanafunzi katika kundi hili hawakuelewa kuwa, mazingira machafu ndio makazi ya wadudu na wanyama hatarishi.

(g) Ni namna gani tunaweza kuwa na mazingira safi?

Katika kipengele hiki mwanafunzi alitakiwa kutambua namna ambayo tunaweza kuwa na mazingira safi. Swali lilikuwa na ufaulu mzuri, kwani wanafunzi wengi waliweza kuandika jibu sahihi ambalo ni *kwa kufanya usafi*. Wanafunzi hao walikuwa na maarifa na ujuzi wa kutambua namna bora ya kuwa na mazingira safi.

Kwa upande mwingine, baadhi ya wanafunzi walienda kinyume na matakwa ya kipengele hiki kwa kuandika *Oksijeni*. Wanafunzi hao walipaswa kuelewa kuwa, mazingira safi hutusaidia kupata hewa safi ya oksijeni. na sio namna ya kutunza mazingira. Vilevile, baadhi ya wanafunzi katika kundi hili walijibu kwa kuandika *shule yetu ina mazingira safi*. Wanafunzi wachache katika kundi hili waliandika, *mazingira machafu ni maficho ya wadudu na wanyama hatarishi kama inzi, mbu, panya na nyoka*. Wanafunzi hao hawakuelewa matakwa ya kipengele hiki. Hivyo walinakili baadhi ya maneno au sentensi kutoka katika kifungu cha habari na kuandika kama majibu. Vielelezo Na. 2.2 na 2.3 vinaonesha mifano ya majibu sahihi na sasiyo sahihi katika swali la 3.

Maswali

- (a) Kwa nini ni muhimu kuishi katika mazingira safi?
kwasababu mazingira safi hupunguza kuenea kwa Magonjwa
mbali limbali kama malaria na kipindupindu.
- (b) Ni kiumbe hai kipi ambacho kina sumu na huweza kudhuru watu na wanyama wengine? Nyoka
- (c) Kwa kuzingatia kifungu cha habari, taja kifaa kimoja kinachotumika kufanya usafi. fyekea
- (d) Ni ugonjwa gani unaweza kuepukwa kwa kufyeka nyasi na kuondoa maji yaliyotuama? Malaria
- (e) Mdudu yupi anaweza kusababisha kuenea kwa ugonjwa wa kipindupindu?
Inzi
- (f) Kutokana na habari uliyoisoma, wadudu na wanyama hatarishi hupatikana wapi? kwenye mazingira Machafu
- (g) Ni namna gani tunaweza kuwa na mazingira safi?
kwakufanya usafi wa mazingira kila siku
na kwaku panda miti

Kielelezo Na. 2.2: Sampuli ya majibu sahihi ya mwanafunzi katika swali la 3

Maswali

- (a) Kwa nini ni muhimu kuishi katika mazingira safi?
Malara
Kipindupindu
- (b) Ni kiumbe hai kipi ambacho kina sumu na huweza kudhuru watu na wanyama wengine? Nyuki inzi Mbu
- (c) Kwa kuzingatia kifungu cha habari, taja kifaa kimoja kinachotumika kufanya usafi. Kufua nyoka kuoya
- (d) Ni ugonjwa gani unaweza kuepukwa kwa kufyeka nyasi na kuondoa maji yaliyotuama? Kufyeka nyasi na kufukia mashimo
- (e) Mdudu yupi anaweza kusababisha kuenea kwa ugonjwa wa kipindupindu? Nyoka ni hatari sana anasumu
- (f) Kutokana na habari uliyoisoma, wadudu na wanyama hatarishi hupatikana wapi? Mbuga za wanyama
- (g) Ni namna gani tunaweza kuwa na mazingira safi?
Mazi kupanda mifyelete
Kufyeka myasimama

Kielelezo Na.2.3: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya Mwanafunzi katika swali la 3

2.2.2 Swali la 4: Kutumia Ramani na Elimu ya Anga katika Maisha ya kila Siku


Swali hili lilitungwa kutoka katika umahiri mkuu wa *Kutumia Ramani na Elimu ya Anga katika Maisha ya kila Siku* na katika umahiri mahususi wa *Kutumia Ramani katika Mazingira*

Yanayomzunguka. Swali hilo lilimtaka mwanafunzi kuchora alama nne za ramani kama swali linavyosomeka;

Chora alama za ramani kuonesha vitu vifuatavyo:

Aina ya Kitu	Alama ya Ramani
(a) Mlima	
(b) Daraja	
(c) Reli	
(d) Kiwanja cha ndege	





Jumla ya wanafunzi 1,545,059 (100%) walijibu swali hili. Kati yao, wanafunzi 80,067 (5.18%) walipata alama zote 8 ambao ni ufaulu mzuri sana, na wanafunzi 264,990 (17.15%) walipata alama 6 ambao ni ufaulu mzuri. Kwa upande mwingine, wanafunzi 547,372 (35.43%) walipata alama 4 ambao ni ufaulu wa wastani. Wanafunzi wengine 652,630 (42.24%) walipata 0 hadi alama 2, ambao ni ufaulu hafifu. Hivyo, ufaulu katika swali hili ulikuwa wa wastani kwani jumla ya wanafunzi 892,429 (57.76%) walipata alama kuanzia 4 hadi 8. Chati Na. 4 inaonesha ufaulu wa wanafunzi katika swali la 4.



Chati Na. 4: *Ufaulu wa wanafunzi katika swali la 4*

Uchambuzi zaidi unadhihirisha kuwa, wanafunzi 80,067 (5.2%) waliopata alama zote 8 walikuwa na maarifa na ujuzi wa kutosha kuhusu *kutambua matumizi ya ramani katika mazingira*. Wanafunzi hao walichora kwa usahihi alama za ramani ambazo ni; *mlima, daraja, reli na kiwanja cha ndege*. Wanafunzi hao walikuwa na ujuzi wa kutosha wa kuchora alama za ramani. Kielelezo Na. 3.1 ni sampuli ya majibu sahihi ya mwanafunzi katika swali la 4.

4. Chora alama za ramani kuonesha vitu vifuatavyo:

Aina ya Kitu	Alama ya Ramani
(a) Mlima	
(b) Daraja	
(c) Reli	
(d) Kiwanja cha ndege.	

Kielelezo Na. 3.1: Sampuli ya majibu sahihi ya mwanafunzi katika swali la 4

Vilevile, wanafunzi 264,990 (17.2%) waliopata alama 6 kwenye swali hili. Wanafunzi hao walichora kwa usahihi alama tatu za ramani kati ya nne zilizotakiwa. Pamoja na hivyo, baadhi ya wanafunzi katika kundi hili walichora alama moja ya ramani isiyo sahihi au, wengine hawakuchora alama mojawapo iliyoulizwa kwenye swali.

Kwa upande mwingine, wanafunzi 900,727 (58.30%) walipata alama kuanzia 2 hadi 4. Wanafunzi hao walidhihirisha uelewa wa wastani katika uchoraji wa alama za ramani. Katika kundi hili,

baadhi ya wanafunzi walichora kwa kuchanganya alama za ramani sahihi mbili na zisizo sahihi mbili. Vivyo hivyo, wanafunzi wachache walichora alama moja sahihi, na alama tatu zisizo sahihi.

Hata hivyo, wanafunzi 286,733 (18.56%) waliopata 0, walikuwa na mapungufu mbalimbali katika uchoraji wa alama za ramani. Baadhi ya wanafunzi waliandika wingi wa alama za ramani ambazo walitakiwa kuchore, kwa mfano, waliandika; *milima, madaraja, reli na viwanja vya ndege*. Wanafunzi wengine katika kundi hili, walichora vitu vinavyopatikana nyumbani kama vile; *mto wa kulalia, mzigo, nyumba, meza na mtu*, ambavyo havikuwa matakwa ya swali. Hii ni uthibitisho kwamba wanafunzi hawa hawakuelewa matakwa ya swali. Vilvile, baadhi ya wanafunzi katika kundi hili walichora *dira* ikionesha pande kuu nne za dunia yaani; *kusini, kazikazini, mashariki na magharibi*. Pamoja hivyo, wanafunzi wengine walichora maumbo ya hesabu kama vile *duara, nusu duara, pembe tatu, mstatili, na mraba*. Majibu ya wanafunzi hawa yanadhihirisha kuwa, hawakuwa mahiri katika kutumia ramani katika mazingira yanayowazunguka. Wanafunzi hao hawakuwa na uelewa kuhusu alama zinazotumika katika ramani kuwasilisha ujumbe kuhusu vipengele na sifa za eneo inayowakilisha katika ramani. Kielelezo Na. 3.2 kinaonesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya mwanafunzi katika swali la 4.

4. Chora alama za ramani kuonesha vitu vifuatavyo:

Aina ya Kitu	Alama ya Ramani
(a) Mlima	Ni watu hupanda na kushuka chini
(b) Daraja	Ni watuwanao ukra kwa mfano chini kuwa mtu
(c) Reli	Ni karabana ambayo ni nyembamba na
(d) Kiwanja cha ndege	Huhua ndege na kushuka watu twe nye ndege

Kielelezo Na: 3.2: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika Swali la 4

Katika Kielelezo Na. 3.2, mwanafunzi katika swali hili amejaribu kuelielezea maana/matumizi ya Mlima, Daraja, Reli na Kiwanja cha ndege badala ya kuchora alama za vitu hivyo.

3.0 TATHIMINI YA UFAULU KWA KILA UMAHIRI

Uchambuzi katika Upimaji wa Darasa la Nne (SFNA) 2023 unaonesha kuwa, kati ya umahiri mkuu wa aina nne uliopimwa (kama ulivyoainishwa kwenye muhtasari wa Elimu ya Msingi wa somo la Maarifa ya Jamii wa mwaka 2016), kiwango cha ufaulu kilikuwa kizuri katika umahiri wa aina mbili. Kiwango cha ufaulu kilikuwa cha wastani katika umahiri mmoja, na hafifu katika

umahiri mwingine mmoja. Umahiri uliofanya vizuri zaidi ni Kutambua Matukio Yanayotokea katika Mazingira Yanayomzunguka ambao ulikuwa na ufaulu wa asilimia 66.83. Umahiri wa Kutumia Ramani na Elimu ya Anga katika Maisha ya Kila Siku ulikuwa na ufaulu wa wastani wa asilimia 57.76. Kwa upande mwingine, kiwango cha ufaulu katika umahiri wa Kufuata Kanuni za Kiuchumi katika Shughuli za Uzalishaji Mali ulikuwa ni wa wastani kwa asilimia 51.79. Umahiri wa Kutambua Misingi ya Uzalendo katika Jamii ulikuwa na ufaulu hafifu wa asilimia 29.79. Ijapokuwa wanafunzi wengi wameweza kupata umahiri unaokubalika katika mahiri tatu, bado wanafunzi hao wana upungufu wa umahiri unaotarajiwa. Kiambatisho cha pekee kinaonesha mchanganuo wa kiwango cha ufaulu katika kila umahiri.

4.0 HITIMISHO

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika maswali ya Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne 2023 katika somo la Maarifa ya Jamii umeonesha kiwango cha ufaulu cha wastani katika umahiri wa aina tatu. Uchambuzi zaidi umeonesha kiwango hafifu katika umahiri wa *Kutambua Misingi ya Uzalendo katika Jamii*. Aidha, kuna changamoto zilizosababisha baadhi ya wanafunzi wasiwe na ufaulu mzuri. Changamoto hizo ni pamoja na kushindwa kuelewa matakwa ya maswali, kukosa maarifa katika dhana zilizopimwa na kushindwa kuwasilisha hoja katika mtiririko mzuri. Hata hivyo, wanafunzi waliokuwa na umahiri waliweza kubaini

majibu sahihi katika maswali yaliyolizwa na hivyo kuwa na utendaji mzuri.

5.0 MAPENDEKEZO

Ili kuboresha kiwango cha ufaulu wa wanafunzi, Baraza la Mitihani la Tanzania linapendekeza mambo yafuatayo:

- (a) Walimu wawaongoze wanafunzi kuchora ramani kwa kuzingatia matumizi ya alama za ramani ili kuwajengea umahiri wa Kutumia Ramani na Elimu ya Anga katika Maisha ya kila siku. Hivyo, kuleta maana katika ujifunzaji.
- (b) Wanafunzi wapatiwe fursa ya kufanya ziara za kimasomo maeneo mbalimbali ya kihistoria, maeneo yanayochimbwa madini ya aina mbalimbali na mbuga za wanyama ili kuwajengea umahiri wa Kutambua Misingi ya Uzalendo Katika Jamii.
- (c) Walimu waanzishe miradi ya vitendo shuleni itakayowawezesha wanafunzi kuelewa dhana kwa undani na hivyo kuwajengea umahiri zaidi katika kutambua matukio yanayotokea katika mazingira yanayomzunguka na katika kufuata kanuni za kiuchumi katika shughuli za uzalishaji mali.
- (d) Wanafunzi wahimizwe kusoma kwa bidii vitabu vya kiada na ziada ili kuongeza maarifa na ujuzi ambao utawawezesha kujibu maswali ya upimaji kwa usahihi.

KIAMBATISHO

03 Maarifa ya Jamii - Ulinganifu wa Ufaulu kwa Wanafunzi katika
kila Umahiri kwa Mwaka 2023 na 2022

NA.	Umahiri	UPIMAJI 2023				UPIMAJI 2022			
		Ufaulu wa kila swali		Wastani wa ufaulu (%)	Maoni	Ufaulu wa kila swali		Wastani wa ufaulu (%)	Maoni
		Namba ya swali	% ya ufaulu			Namba ya swali	% ya a ufaulu		
1	Kutambua Misingi ya Uzalendo Katika Jamii	2	29.79	29.79	Hafifu	1	74.34	74.34	Mzuri
2	Kutambua Matukio Yanayotokea Katika Mazingira Yanayomzunguka	3	66.83	66.83	Wastani	2	72.46	72.46	Mzuri
3	Kufuata Kanuni za Kiuchumi Katika Shughuli za Uzalishaji Mali	1	51.76	51.76	Wastani	3	44.77	44.77	Wastani
4	Kutumia Ramani na Elimu ya Anga Katika Maisha ya Kila Siku	4	57.76	57.76	Wastani	4	26.25	26.25	Hafifu

